# OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Barua pepe: masanzesecondaryschool@gmail.com
Simu: 0714070790/0694201510

SHULE YA SEKONDARI MASANZE,
S.L.P. 130,
**KILOSA.**

KUMB. NA/MSS/SA.20/JISR/_______ **TAREHE:** ___/___/2021

JINA LA MWANAFUNZI ________________________________________________

S.L.P. _______________

____________________

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASANZE WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021.</u>**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule ya sekondari Masanze mwaka 2021. Shule ya sekondari Masanze ipo umbali wa Kilomita 14, kutoka Makao makuu ya Wilaya Kilosa (Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa). Shule ipo umbali wa Takribani Kilomita 2 kutokea barabara kuu ya kuelekea Mikumi kuanzia Kituo cha mabasi cha Miyombo, Kilichopo Kata ya Masanze. Nauli ni Shilingi 2,000/= kwa basi zinazoelekea Mikumi kutokea stendi ya Uhindini.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021, mwanafunzi anatakiwa kufika bial kukosa shule tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 22/01/2021 ndani ya wiki mbili (siku 14) baada ya tarehe ya kuripoti shuleni.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

### A: SARE YA SHULE(MPYA)

#### (i) Wavulana:

- Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi **aina ya Tomato** yasiyobana.
- Suruali mbili (2) za **rangi ya damu ya mzee** zenye Marinda mawili kila upande, upana wa miguu iwe nchi kumi na sita (16). (Kitambaa Maruni estim No.1)
- Viatu vyeusi vya Ngozi visivyochongoka vya kamba na **SIYO RABA NYEUSI**
- Soksi Nyeupe
- Mkanda Mweusi wa ngozi wenye Kichuma cha kawaida cha kufungia
- Sweta la Damu ya Mzee (Maruni)
- Tai za rangi ya damu ya mzee zenye mistari mieupe ya Pundamilia mshazari
- Tisheti ya shule aina ya Form six rangi ya Blue Bahari
- Sare za michezo za trak/ rangi ya blue na t-shert rangi ya blue pamoja na raba nyeupe.

### (ii) Wasichana:

- Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi **aina ya Tomato** yasiyobana.
- Sketi mbili (2) za **rangi ya damu ya mzee** (Maruni), mshono wa rinda box. Iwe ndefu kufikia vifundo vya miguu. Belti yake iwe nchi moja na nusu (1½) na iwe pana isiyobana mwili. (Kitambaa Maruni estim No.1)
- Viatu vyeusi vya Ngozi vyenye kamba visivyo na visigino virefu na **SIYO RABA NYEUSI**
- Soksi Nyeupe
- Sweta la Damu ya Mzee (Maruni)
- Kwa wanafunzi wa Kiislam nusu kanzu yenye mikono mirefu, Hijabu pana na ndefu yenye kufunika mikono. Rangi ya Hijabu iwe nyeupe.
- Tai za rangi ya damu ya mzee zenye mistari mieupe ya Pundamilia mshazari
- Tisheti ya shule aina ya Form six rangi ya Blue Bahari
- Sare za michezo za trak/rangi ya blue na t-shert rangi ya blue pamoja na raba nyeupe.

**NB:** -Tisheti ya shule ni sare ya shule kama zilivyo sare zingine ni lazima kila mwanafunzi Awe nayo.
-Si vyema kumnunulia mwanafunzi sare za mwanafunzi aliyemaliza. Ukaguzi wa vifaa na sare utafanyika siku mwanafunzi atakaporipoti.

### B: VIFAA VYA DARASANI

- Daftari Kubwa tisa (09) (Counter books)
- Mkebe wa Hesabu (Mathematical Set) na rula sentimeter 30.
- Kalamu za wino (Blue or Black) na Penseli
- Daftari tisa (09) ndogo za msomi
- Kamusi ya Kingereza na Kiswahili
- Vitabu vya masomo mbalimbali atakayosoma
- Begi Imara la Kubebea Vifaa vyake vya Shule na SI MFUKO.

### C: CHAKULA CHA MCHANA

- Chakula cha mchana cha wanafunzi, wazazi wanachangia kupitia kamati ya wazazi waliochaguliwa kupitia vikao vya wazazi shuleni.

### D: USAFI NA MAZINGIRA

- Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na mche wa mti mmoja wa matunda uliooteshwa kwenye kiriba chake uliokuwa na Afya.
- Pia aje na Vifaa vyake vya kufanyia Usafi

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII NI:-

### (A) MWENENDO UNAOPASWA KUUFUATWA

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu No. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria No. 10 ya mwaka 1995. Pia inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Teknolojia pamoja na Miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

**Hivyo,** unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa zaidi na kupewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudurio mazuri na kamilifu katika kila shughuli zote ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili na malazi na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare za Shule kamilifu wakati wote unapokuwa katika mazingira ya Shule.
h. Mwanafunzi aepuke vitendo viovu kama vile; matusi, utoro, wizi, ugomvi, ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya, uvutaji sigara/bangi, uasherati, ushoga, kuoa au kuolewa, kutoa Mimba, Kusababisha mimba, Kushawishi kutoa mimba, Kuchochea Migomo na Kuvuruga Amani ya Shule.
i. Mwanafunzi hapaswi kuvaa urembo wa aina Yoyote kama vile Hereni, Mkufu, Bangili, Pete, kupaka rangi kucha au Midomo, kuwa na kucha ndefu, Kutia dawa nywele au kuchora Tatoo sehemu yoyote ya mwili wake.
j. Pia mwanafunzi hatakiwi kutembelea nyumba za kulala wageni, kumbi za starehe kama vile Disco, Vigodoro, Mabanda ya Video na Maeneo wanayocheza POOL TABLE.
k. Mwanafunzi haruhusiwi kufuga ndevu, kuwa na nywele ndefu au Kunyoa Mitindo isiyoruhusiwa.
l. Mwanafunzi hapaswi kuwa na Simu ya Mkononi, sim card wala vocha awapo Shuleni na Akikutwa navyo vitachukuliwa na Havitorudishwa.
m. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
n. Mwanafunzi ni lazima aheshimu bendera na wmbo wa Taifa
o. Mwanafunzi analazimika kutunza mali binafsi na za Umma. Pia Kuepuka kuchora au kuandika katika vitabu vya shule, Kuta, madawati, Viti, meza na Mbao za Kufundishia. (uharibifu wowote wa mali za Shule atawajibika kuulipa).
p. Mwanafunzi hapaswi kufanya biashara zozote katika maeneo ya shule.

**(B) MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUZWE SHULE.**

a. Wizi wa aina yeyote ile.
b. Uasherati, ubakaji na ushoga
c. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
d. Uvutaji sigara na bangi
e. Makosa ya jinai
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g. Kudharau Bendera ya Taifa
h. Kuoa au kuolewa
i. Kupata mimba au kushawishi kutoa mimba
j. Kutoa mimba au kushawishi kutoa mimba
k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani au usalama wa shule au watu.
l. Kukataa adhabu kwa makusudi
m. Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 **Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa na wanafunzi shuleni**

a. Kuja na picha (4) za pasipoti size
b. Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara atakaporipoti shule.
c. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai, form hii nayo utaikabidhi kwa mkuu wa shule.
d. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, Kanuni, Taratibu na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.

**TANBIHI:** Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu KARIBU SANA MASANZE SEKONDARI!!!.

**GODWIN T. MOSHA**
**MKUU WA SHULE**

**KIAMBATANISHO A: FOMU YA KUMWANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI MASANZE**

**(Jaza fomu hii kwa uangalifu)**

Picha ya Mwanafunzi

1. Jina kamili la Mwanafunzi ____________________________________________
2. Tarehe ya kuzaliwa __________ Wilaya alipozaliwa _____________Uraia__________
3. Kabila ____________________Uraia ______________Dini ____________________
4. Jina la Mzazi ____________________________Simu ya Mzazi: ___________________

   Anwani ya Mzazi ____________________ Kazi ya Mzazi ______________________
5. (Sehemu hii ya 5 ijazwe na wanafunzi ambao hawana wazazi wao YAANI YATIMA)

   (a) Jina la Mlezi ________________________ Simu No: ________________

   (b) Uhusiano kati ya Mlezi na Mwanafunzi: ____________________________

   (c) Kazi ya Mlezi: ___________________ Anwani ya Mlezi ______________________
6. Wakati wa likizo mwanafunzi atakwenda wapi? ____________________________
7. UKIRI WA MWANAFUNZI KUKUBALI KUSOMA NA KUFUATA SHERIA ZA SHULE

   Mimi_____________________________ nimesoma na Kuyaelewa vyema Maelekezo yote ya Shule ya Sekondari Masanze. Hivyo nakubali kuipokea nafasi hii ya Masomo niliyopewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ninaahidi Kusoma kwa Bidii ili niweze kufaulu, kuwa na Maisha Bora na Kuwa Raia mwema, Mzalendo nitakayeipenda na Kuijenga Nchi yangu ya TANZANIA. Ninafahamu kwamba, Ili kuyaandaa maisha yangu ninapaswa Kujali sana Elimu na Kusoma kwabidii. Hivyo nikiwa na akili zangu timamu niaahidi kufuata Sheria,taratibu na Kanuni za Shule Kikamilifu. Naomba Mwenyezi Mungu anisaidie.

   Saini:___________________ Tarehe:______________
8. UKIRI WA MZAZI/MLEZI

   Mimi _______________________ nimehakikisha mwanangu amezisoma na kuzielewa Sheria na Taratibu za Shule. Nimemsisitiza pia Kuzizingatia na kufuata Lengo la Kusoma kwa bidii. Pia naahidi Kumhudumia mwanangu mahitaji yake ya Elimu na Kushirikiana na Walimu katika Kufanikisha safari ya Mwanangu katika kupata Elimu. Naomba Mwenyezi Mungu anisaidie.

   Saini:___________________ Tarehe:______________

## APPENDEX C: MEDICAL EXAMINATION REPORT

Barua pepe: masanzesecondaryschool@gmail.com
Simu: 0714070790/0694201510

SHULE YA SEKONDARI MASANZE,
S.L.P. 130,
**KILOSA.**

KUMB. NA/MSS/SA.20/JISR/________ **TAREHE: ______________**

## PART A: EXAMINATION DETAILS

MR./MISS ____________________________________________

Please Examine the above named student as to his/her Physical and Mental fitness for full time student in this School. The Examination should include the following:

1. Haemoglobin……………………………………………………………………………………
2. P.V Bleeding ……………………………………………………………………………………
3. Sight………………………………………………………………………………………………
4. Blood Pressure …………………………………………………………………………………
5. Urine for Sugar…………………………………………………………………………………
6. Stool for Routine Examination……………………………………………………………...
7. Pregnancy Test …………………………………………………………………………………
8. Skin Diseases ……………………………………………………………………………………
9. Leprosy …………………………………………………………………………………………..
10. Any Deformity …………………………………………………………………………………
11. COVID 19………………………………………………………………………………………
12. Epilepsy …………………………………………………………………………………………
13. Pulmonary Tuberculosis ……………………………………………………………………
14. Neurosis …………………………………………………………………………………………
15. Venereal Diseases ……………………………………………………………………………
16. Other Serious Diseases ………………………………………………………………………

## PART B: CONFIRMATION BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER

1. I have examined the above named Student and considered that He/She is Physically fit/ Unfit for a Full time Schooling.
2. Other comments……………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………………
3. Name: ………………………………………… Station:……………………………………………..
   Designation: ……………………………. Signature:…………………………. Date:……………..
   Official Stamp: